# Tathmini ya Binadamu na Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto*

*Waithiru Kago Antony*
*Chuo Kikuu cha Laikipia*

**Ikisiri**

**Makala haya yalinuia kudhihirisha jinsi binadamu huingiliana na mazingira yake katika riwaya ya *Nakuruto* ya mwandishi maarufu – Clara Momanyi – na mwenye mwelekeo chanya dhidi ya mazingira kama inavyodhihirika katika matini yake. Uhakiki huu uliongozwa na baadhi ya nguzo kuu za nadharia ya uhakikimazingira, kama vile, utamaduni na maumbile, binadamu dhidi ya maumbile, maadili ya mazingira, baina ya zingine kadhaa. Momanyi aliandika matini ya *Nakuruto* wakati ambapo kazi za fasihi ya kimazingira zilikuwa haba. Binadamu katika shughuli zake za kila siku, huweza aidha kuyatunza au kuyachafua mazingira. Mara nyingi ni uchafuzi ambao hutekezwa zaidi kuliko uhifadhi. Hili lilidhihirishwa na tathmini hii, ambapo ilibainika kuwa mwanadamu amekuwa akiyapuuza mazingira, lakini jinsi muda unavyosonga mbele ndivyo ameanza kumakinikia na kuajibikia mazingira. Uajibikaji huu umeimarisha uhifadhi wa mazingira kama inavyodhihirika katika riwaya ya *Nakuruto.* Uhakikimazingira ni usomi wa fasihi na mazingira kwa kujikita katika mwelekeo unaohusu maeneo ya taaluma zaidi ya moja. Hivyo, kwa msingi huu, makala haya yaliafikia kutathmini matini ya *Nakuruto* ambayo ina masuala ya kimazingira na kujaribu kumaizi jinsi ambavyo Momanyi amedhihirisha mchango wa binadamu katika mazingira kisanaa.**

**Maneno Muhimu:** Binadamu, Mazingira, Uhakikimazingira, Maadili ya Mazingira, Maumbile.

**Utangulizi**

Riwaya kama tanzu zingine za fasihi, hubuniwa kwa lengo mahususi na hasa maalumu kwa binadamu (Nayar 2010). Fani na maudhui ni vipengele pacha ambavyo ni msingi katika kazi yoyote ya fasihi. Ingawa mtindo wa mwandishi fulani hutawaliwa na maarifa, mazingira alimokulia na au ya uandishi pamoja na tajriba mbalimbali, mtindo huathiri upangaji na matumizi na usanii wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi (Wamitila 2010; Ntarangwi 2004). Makala haya yameshughulikia maingiliano kati ya binadamu na mazingira kama yalivyosanwa na Momanyi kupitia vipengele vya kimtindo mbalimbali katika misingi ya kimazingira. Mazingira huweza kufafanuliwa kama hali, mimea, bidhaa au vifaa vinavyoyazunguka maisha ya kiumbe. Baadhi ya vitu ambavyo humzingira kiumbe yeyote yule ni pamoja na wanyama, watu, mimea, maumbile, maji, hewa, na vingine vingi ulimwenguni (Robert na Christine 2016).

Kwa mujibu wa Morton (2012) akimnukuu Glotfelty (1996), taaluma ya fasihi ya mazingira ni dhana ambayo ilichipuka katika miaka ya themanini kisha ikashamiri katika miaka ya tisini. Lengo kuu la taaluma hii katika fasihi huwa kuongeza kanoni ya fasihi ya mazingira pamoja na usomi wa tamaduni mbalimbali na mchango wazo katika mazingira. Morton anasisitiza kuwa, kushamiri huku kulichangiwa na haja ya kutathmini nafasi ya fasihi katika uhifadhi wa mazingira, hasa katika kipindi hiki cha utandawazi, maendeleo endelevu, na teknolojia ya kisasa. Isitoshe, anaamini kuwa, fasihi ina nafasi kubwa katika harakati za uhifadhi wa mazingira. Aidha, anabisha kuwa, fasihi kama ala inaweza kutumiwa kudhibiti upujufu wa mazingira kwa kuihamasisha na kuielimisha jamii kuhusu athari hasi za mazingira chafu. Bulaya na Mhango (2022) wanaeleza kuwa, fasihi imefanikiwa kwa njia moja au nyingine kuwaelimisha na kuwahamasisha wanajamii kuhusu haja ya kuyatunza mazingira ili kuepuka maangamizi. Kadhalika, wanasema kuwa, nadharia ya uhakikimazingira hutumiwa kuchambua kazi za kifasihi na sanaa kwa kujikita katika misingi ya uhusiano au na muumano na wakati mwingine utegemeano kati ya binadamu na ekolojia. Kimsingi, fasihi hutumia lugha kwa usanii katika kuangazia changamoto zinazoikumba jamii kimwavuli (Garrard 2004).

Momanyi kupitia mhusika Nakuruto katika riwaya yake ya *Nakuruto* anaashiria jinsi ameshuhudia manufaa ya mazingira nadhifu na mema. Mathalani, anakiri kuwa mazingira mema huhakikishia jamii shibe, upendo, umoja na maendeleo endelevu. Hata hivyo, majirio ya Mnguzu yanazalisha kukauka kwa visima, kuchipuka kwa chuki baina ya wanajamii, ukame na hatimaye maafa ya watu na wanyama. Chanzo kuu cha dhiki hizi ni umangimeza kama anavyoeleza mwandishi ambao unayafanya maisha ya wanajamii kuwa magumu na kuyatamausha. Momanyi anadhihirisha jinsi ubinafsi wa mabwanyenye wachache unavyozalisha upujufu wa mazingira na kisha maafa kutokana na athari hasi. Athari hizi hupaliliwa na ubinafsi, ufisadi na uongozi mbaya katika kipindi cha utandawazi.

**Utamaduni na Maumbile**

Utamaduni ni mseto wa mila, itikadi, jadi, desturi na chimbuko la jamii fulani (TUKI, 2013). Kimsingi, kila jamii huwa na utamaduni ambao huiwezesha kuhifadhi mazingira kupitia njia mbalimbali. Mathalani, mhusika Nakuruto anafafanua kuhusu utamaduni uliohusisha utoaji wa kafara kwa miungu ili mvua iweze kunyesha. Heise (2016) anadai kwamba, fasihi ina uwezo wa kuimarisha utamaduni mwafaka kwa jamii na mazingira kwa jumla. Bulaya na Mhango (2022) wanakiri kuwa, utamaduni wa jamii huwa na fursa ya kipekee, pana na ya kina katika ujenzi wa mtazamo na mielekeo inayoathiri matumizi ya mazingira kwa njia mbalimbali. Ukame ulipoikumba nchi na kusababisha maafa kutokana na njaa, wazee walikuwa wakitoa sadaka ya msichana aliyekuwa mrembo zaidi kijijini. Punde tu walipotoa kafara hiyo kwa miungu, mvua iliweza kunyesha na wenyeji wakavuna vyakula hadi maghala ya kuvihifadhia yakatapika. Ijapokuwa kuna muda ambapo ajuza mmoja alikiuka desturi na kumwokoa mjukuu wake mrembo kutokana na kutolewa kafara, aliwatuliza nyoyo miungu kwa kuwashonea uteo uliosheheni shanga za rangi mbalimbali. Ajuza aliutarizia mapambo ya kitamaduni ili ukubaliwe na miungu badala ya mjukuu wake na bila yeyote kujua, alimwokoa mjukuu wake na pahala pake akawapa miungu uteo. Ukosefu wa mvua ulisababisha maafa kwa sababu chakula kiliadimika kabisa. Wamama wachanga walikuwa wakiteleka vyungu na kuyachemsha mawe ili kuwapa imani watoto kuwa chakula kilikuwa mekoni hadi pale walipolala kando ya meko. Hivyo, utamaduni ulitumika kuhifadhi na kuyapa uhai mazingira.

Kwa upande mwingine, maumbile huwa umbo la asili la viumbe katika mazingira halisi ya kubuni katika kazi za sanaa na fasihi (TUKI 2013). Kwa mujibu wa nguzo hii, mimea, wanyama, wadudu na ndege mbalimbali huweza kuupamba ulimwengu na kuyafanya mazingira yavutie. Hivyo basi, kinachohitajika ni urari kati ya hali za kimaumbile uwepo. Urari huu husaidia kuchangia na kukamilisha mfumo mzima wa ekolojia (Kusserow 2018). Momanyi kupitia mhusika Nakuruto anadhihirisha na kuunga mkono mhimili huu pale anaposawiri mbuga iliyokuwa na nyasi ndefu na mito iliyopindana kwa madaha ikielekea isikokujua. Anaeleza kuwa, mara kwa mara mito ile iliulizana njia na ilipopotosha ilibishana yenyewe kwa yenyewe. Mle mna miti, mimea, ng'ombe waliolishwa na wachungaji, kondoo, mbuzi na ndama mtawalia. Wachungaji walivalia shuka huku wakining'iniza vibuyu na viriba vya maji shingoni, pamoja na pote za pinde zilizong'ang'ania mabegani na mariaka yaliyosheheni mishale yalining'inia migongoni pia. Hili ladhihirisha urari kati ya hali za kimaumbile (uk. 6 – 7).

**Binadamu Dhidi ya Maumbile**

Binadamu huwa na uhusiano wa kisimbiotiki kati yake na maumbile yanayomzingira katika janibu anazoishi na kutawala. Morton (2012) anadai kuwa, uhakikimazingira humulika uhusiano uliopo baina ya binadamu, wanyama, maumbile na ekolojia asilia. Mathalani, anasema kuwa, binadamu na mazingira huweza kuwa na uhusiano wa kisimbiotiki. Hii ni kwa sababu, binadamu na mimea hutegemeana katika kuzalisha gesi ya kupumua. Hivyo, uharibifu wa mazingira ni tishio kwa uhai wa binadamu. Mathalani, Bi. Kizee mmoja aliyejikongoja akielekea kwenye ziwa ambalo chanzo chake kilikuwa mauzauza, alikutana na mzee Mngolia. Mzee Mngolia alimtahadharisha dhidi ya kuelekea kwenye ziwa lile licha ya kuwa lilisheheni maji maangavu yaliyometameta juani pamoja na maelfu ya samaki. Bi. Kizee yule alimjuza mzee Mngolia kuwa ziwa lile lingeitwa Nakuruto na kuwa lingeirutubisha nchi yao na kuijaza shibe. Alimhimiza mzee Mngolia kuwa, walitunze ziwa lile zaidi

ya mama mzazi ambaye humtunza mwanawe. Hii ni kwa sababu, kulingana na Bi. Kizee, ndani mwa ziwa lile mlikuwa uhai wa akina mzee Mngolia na wananchi wa eneo lile.

Momanyi katika *Nakuruto* anasema kuwa maji ni pumzi ya uhai kwa binadamu na kuwa ardhi ni kitovu cha uhai. Kadhalika, kupitia mhusika Nakuruto anasisitiza umuhimu wa kuhifadhi mazingira, hasa vitovu vya maji. Mathalani, anasema kuwa ziwa liitwalo Ipe ndilo chanzo cha mwendelezo wa uhai wa wanakijiji. Hata hivyo, wanakijiji kama vile Ludao wanajizatiti kuukatiza uhai wao. Umati wa wanawake na watoto pia hawakuachwa nyuma katika harakati za kuliangamiza ziwa Ipe kwa kuchafua mazingira yake. Umati ule ulikuwa ukifua nguo pale kando ya ziwa na kuendelea kuchafua ziwa lile. Aidha, maji taka yalikuwa yakimiminiwa ziwani kwa fujo. Povu la sabuni lililomwagwa pale kwa muda mrefu tayari lilikuwa limeathiri mazingira ya ziwa. Kwa mujibu wa Momanyi, uchafuzi wa mazingira huzalisha athari hasi kwa mazingira na viumbe kwa jumla. Kwa mfano, miti iliyokuwa karibu na ziwa Ipe, ilikuwa imeanza kupiga manjano kutokana na magadi mengi ya sabuni iliyotokana na ufuaji nguo pale.

Nayar (2010) anaungama kuwa binadamu hujibidiisha kuharibu mazingira kisha hujutia athari zake baadaye. Kwa mfano, pale kando kidogo karibu na ziwa Ipe, wanawake wengine walikuwa wakiteka maji huku wengine wakioga bila kujali athari za matendo yao. Matendo haya ya uharibifu bila kujali yalisababisha kushamiri kwa gugumaji lililokuwa likimenyelea tena taratibu, huku likifunika uso wa ziwa Ipe. Hili lilipelekea kutishiwa uhai wa wanakijiji ambao ndio waliokuwa chanzo cha upunjufu wa mazingira yale. Ziwa Ipe lilikuwa mshipa wa uhai wa Waipe na kukauka kwa ziwa kuliashiria maangamizi kwa Waipe kwa jumla. Nakuruto aliwakumbusha Waipe kuwa, hasara humfika mwenye mabezo na mapuuza. Hii ni kwa sababu, Waipe walikuwa wanahatarisha maisha yao kwa kulichafua ziwa Ipe. Ziwa hili lilisitiriwa na mto mmoja tu na hamkuwa na chemichemi wala vijito vilivyolilisha ziwa lile. Wakulima walichangia pakubwa kutishia uhai wa Waipe. Walizidi kuchimba mitaro mikubwa ya kupitishia maji ya ziwa mashambani mwao, jambo ambalo lilitishia kukauka kwa ziwa.

**Uongozi Mbaya na Maendeleo Endelevu**

Uongozi mbaya au utawala dhalimu unaposhamiri, mazingira huchafuliwa kwa kiwango kikubwa sana. Hata hivyo, utawala dhalimu unapofifia mazingira huweza kuchipuza na hili huzalisha uchipuzi wa uhai wa jamii kimwavuli (Nayar 2010 na Mwaniki 2019). Waithiru (2019) anafafanua kuwa, maendeleo endelevu ni mchakato unaohusisha utawala na uongozi mwema pamoja na uwajibikaji wenye maadili dhidi ya rasilimali na usawa wa kimazingira. Maadili mema katika ugavi wa rasilimali na katika maingiliano na mazingira huchangia pakubwa katika maendeleo endelevu. Momanyi akimuunga mkono anashadidia kauli kuwa, baada ya utawala wa manyanyaso ulipoanguka watu waligawanya shamba na kubomoa kuta zilizojengwa kando ya mto ili kuwazuia kutumia maji ya mto Milu. Ikizingatiwa kwamba maji ni kitovu cha uhai kwa watu, tendo la Bw. Brook kubinafsisha mto na kuwanyima Walatimbi maji ni ishara ya maangamizi. Ndiposa mwandishi anakiri kuwa:

> Kijiji cha Latimbi kikavuma tena kwa uhai mpya. Mashamba yalilimwa na mimea anuwai kukuzwa. … Mvua za neema zikanyesha na kijiji kikanawiri. Mto Milu ukavuma kwa wingi wa maji ambayo awali yalifujwa na dhalimu yule. Walatimbi walivuna vyakula wakavijaza kwenye maghala hadi vingine vikawa vinaoza na kuozeana shambani …. Kwa kadri miti ilivyochipua uhai, ndivyo watu walivyochipuza kizazi kilichokita mizizi katika uasili wa mazingira yao (uk. 50).

Kadhalika, uongozi mbaya huzalisha sera mbovu zinazochangia uzorotaji wa mazingira. Mathalani, wakaaji wa Maweni waligubikwa na ulofa kutokana na sera za watawala zilizopalilia ubinafsi mkubwa. Sera mbovu zilizalisha uharibifu wa mali asili na kufujwa kwa ardhi hadi ikawa yabisi na wanyonyaji. Mtawala kutoka nchi ya Wanguzu aliwahamisha wanakijiji ili kutoa nafasi kwa uchimbaji madini kwa lengo la kujitajirisha mwenyewe. Kwa mujibu wa mzee Saluda, wanakijiji walihamishiwa kwenye ardhi kame na tasa iliyojaa mawe, kokoto na miamba si haba. Eneo lile halikuweza kuzalisha chakula na hili lilisababisha kudhoofika na kufukarika kwa Wamaweni. Aidha, mifugo wao waliaga kutokana na ukame na mazingira walimohamia yakachafuka kutokana na

msongamano wa vibanda. Ingawa ukataji miti na uuzaji wa mchanga vilichangia ulofa, kiini kilikuwa uongozi mbaya. Mzee Saluda anaeleza kuwa, kutokana na hali mbaya ya uchumi, wanakijiji walilazimika kukata miti na kuichoma makaa yote. Jambo hili lilisababisha ukosefu wa mvua na hatimaye, ukame. Baada ya kumaliza miti, waliteka mchanga na kuwauzia wajenzi wa makasri.

Kutokana na haja ya maendeleo, wanakijiji walihama ili kutoa nafasi ya uchimbaji madini. Maeneo waliyohamia yakawa jangwa na walimohama yakasheheni mtaa wa wakwasi, makabaila na wanyonyaji waliofaidi madini bila kuwajali wanakijiji. Mabwanyenye wale walihonyoa mali ya wanakijiji huku wakipuuzilia uhai wao mbali. Aidha, walisafirisha madini ughaibuni na kujitajirisha wenyewe. Tamaa na ubinafsi wa watawala ilisababisha maafa kwa wachochole ambao walikuwa watumwa hasa. Mzee Saluda anahuzunika anapoteta kuwa:

> Machimbo hayo yamepoteza watoto wetu wengi mno mama. Wengine wameangukiwa na majabali humo wakazikwa wakiwa hai. Wengine wamezirai humo kutokana na ukosefu wa hewa ya kutosha na wengine mvua zikanyesha, mashimo yakajaa maji na kuwazamisha kabisa (uk. 60).

Viwanda vilivyojengwa na Wanguzu pale Maweni vilizalisha athari chungu nzima hasi kwa wenyeji. Mzee Saluda alidai kwamba hewa ya sumu iliyozalishwa na viwanda ilisababisha vifo vya watu, wakiwemo watoto. Maangamizi ya watoto yaliashiria hatima ya kizazi cha siku za usoni. Hili ni jambo la huzuni na mafadhaiko kwa jamii. Walioathirika mle viwandani walitanguliza kwa kukohoa. Kisha walitatizika kupumua na hatimaye, walizirai na kufariki. Baadhi ya wanakijiji walioaga ni kama vile mtoto wa mzee Menga. Hivyo, maendeleo yanapelekea hasara zaidi kuliko manufaa kwa wanakijiji.

Uongozi mbaya unachangia uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa. Mathalani, wakati Nakuruto na Leboni walipokuwa kwenye mkahawa uitwao *Vivid Dreams Restaurant* aliwasikia wanaume watatu wenye vitambi na waliovalia nadhifu wakipanga njama ya kuwafurusha watu kutoka kwenye ardhi yao. Katika gumzo lao, mmoja wao alikiri kuwa ardhi hiyo ingekuwa yao baada ya wenyeji kufurushwa. Hata hivyo, mna mmoja baina yao mwenye utu. Ni yeye tu aliyewajalia wananchi walioishi pale. Aidha, anawauliza wenzake: 'Mnh, wale jamaa wataenda wapi, na wengi wana watoto?' (uk 87). Kadhalika, watoto wa shule ya msingi ya Majaaliwa walikuwa wanaendelea na masomo yao chini ya mti wa mbuyu. Chanzo cha wao kufurushwa ni tajiri mmoja aliyedai kuwa shule ile ilijengwa katika ploti yake. Sababu ya kutimuliwa ni ubinafsi, tamaa na ufisadi ambao ni watoto wa uongozi dhalimu.

Shule ya Majaaliwa ilizungushiwa seng'eng'e na lango hulindwa na askari wawili wakisaidiwa na majibwa makali yenye meno makali. Bw. Mabavu bin Mahela alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wamefaidi harufu ya nta ya Quick Buck. Hili laashiria uongozi mbaya ambao baada ya Mbeberu kuondoka uliendeleza mbinu mbovu za uongozi. Nta inaashiria uwezo, mamlaka na utajiri unaomilikiwa na mataifa tajiri ya Uropa, Ulaya, Asia, Marekani na mengine mengi yanayooza kwa utajiri. Mataifa tajiri yanayakopesha mataifa fukara ya Afrika na kisha kuyatoza riba ya juu zaidi, jambo ambalo huwapelekea Waafrika kuwa watumwa. Kwa upande mwingine, mji mkuu wa Maboni unaashiria mataifa fukara ya Afrika yanayotegemea mataifa tajiri ya kigeni kujiendeleza na kujitawala. Uongozi mbaya umechangia watoto kusomea ndani ya mahema katika baadhi ya mitaa, mjini Maboni. Hali hii inapaliliwa na unyakuzi wa ardhi ya umma. Viongozi wenye tamaa na ubinafsi wanataka kujinufaisha wao bila kujali wananchi. Wananchi wale wale wanakuwa wakimbizi katika taifa lao.

Majengo ya wananchi yanabomolewa pamoja na majengo ya shule. Jambo hili linatatiza shughuli za masomo katika maeneo yale pamoja na kutatiza maisha kwa jumla. Kwa mfano, Leboni anaeleza kuwa matingatinga yalitumiwa kubomoa majengo ya shule, hali iliyosababisha watoto kusomea ndani ya mahema. Mahema yenyewe walitunukiwa na wahisani waliowaonea huruma ili angaa wajikinge na dhoruba kali za jua na mvua. Aidha, majengo yote ya maabadi yanavuma umati wa wakimbizi kutoka vijiji jirani. Kwa misingi hii hii, uongozi dhalimu unazalisha wakimbizi kwa idadi kubwa. Viongozi wanaoongozwa na tamaa wanachoma makazi ya watu mbalimbali na kupelekea umati mkubwa wa

watu pamoja na mifugo kukosa makao na hivyo walikimbia kuelekea wasikokujua. Kwa mfano, vigogo wanawachomea wenyeji nyumba na vitu vyao. Nakuruto anafadhaika sana anapotazama nyuma ulikotokea umati wa watu na mifugo na kuona moshi mkubwa uliotanda na kufanya wingu jeusi lililoenea kama blanketi katika eneo lile.

**Utandawazi**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 331), "Utandawazi ni dhana inayotumiwa kuelezea mikabala ya kiutamaduni na hata kisiasa ambayo inasisitiza muungano na mahusiano yanayokiuka mipaka ya taifa-dola. Huhusisha pia kani za kimazingira." Kupitia mhusika Nakuruto, Momanyi anafafanua kuwa, Wanguzu walisaki inda na ubinafsi. Wanguzu wanaashiria wakoloni ilhali Wamaweni wanaashiria Waafrika. Wanakijiji waliwaogopa Wanguzu. Kwa mfano, mzee Saluda anakiri kuwa,

> "…Kila akohoapo haini mmoja watu humkimbilia kutaka kujua shida yake hata wengine kujikwaa ovyo" (uk. 60). Zaidi ya hayo, anaongeza kuwa Wanguzu waliwanyima Wamaweni fursa za ajira. Kwamba, watoto wa pale Maweni waliohitimu taaluma tofauti tofauti walinyimwa ajira na itokeapo kwamba wamebahatika, zilikuwa kazi za aibu kusimulia. Mzee Saluda alishangaa ikiwa Maweni hapakuwa na matarishi, makarani au hata wafagiaji, hivi iwe lazima wangetoka ughaibuni.

Aidha, Wamaweni hawana cha kujivunia. Hii ni kwa sababu, walisalia kuwa maboi tu majumbani mwa Wanguzu; wapagazi wa kubeba shehena za bidhaa zao; wachimbaji madini kwenye mgodi ulio katika ardhi ya Wamaweni na matopati tu. Mfumwa ambaye ni ishara ya viongozi dhalimu katika mataifa mengi barani Afrika anaungana na Wakoloni kuwanyanyasa wananchi. Mateso haya hufanikishwa kupitia utawala wa Waafrika na Wanguzu kupitia viongozi Waafrika ambao ni vikaragosi vya Ulaya na Uropa. Hili linadhihirishwa na mzee Saluda anapokariri kuwa, "Inaonekana wewe ni jasusi, kibaraka wa wale Wanguzu kama huyo mzee wa kijiji tu" (uk. 61). Kutokana na utandawazi, wenyeji wa Maweni wanaishi katika ardhi kame na yabisi mithili ya tumbo la tasa. Walisukumwa na Wanguzu hadi ukingoni mwa maangamizi wakaharibu udongo uliohimili uzao wao tangu 'ndemi na mathathi'. Hata hivyo, Nakuruto anawapa matumaini ya mabadiliko mema. Viongozi wengi wa mataifa fukara barani Afrika hujijali wao binafsi bila kujali matatizo yanayowakumba wananchi. Mathalani, kutokana na tamaa na ubinafsi wa Bw. Mfumwa – mzee wa kijiji cha Maweni – Wanguzu kama Wellingtone waliendeleza unyonyaji, usaliti na unajisi wa mazingira bila usumbufu. Aidha, alimuenzi Mnguzu Wellingtone kiasi cha kumpigia magoti kwa sababu uhusiano wake naye ulimfaidi sana yeye binafsi.

Baada ya Wamaweni kuwafukuza Wanguzu na kujitawala wao dhiki ziliwavamia kwa mpigo. Hii ni kwa sababu, Wanguzu hawakuwapa fursa ya kujifunza mbinu za kuzalisha mali seuze za kuendesha biashara na viwanda mbalimbali. Ulitima ulishamiri na kunawiri si haba. Tatizo kubwa kwa wenyeji wa Maweni lilikuwa maji. Wanguzu waliharibu mifereji yote ya maji punde tu Wamaweni walipowagomea. Maweni mlibakia kisima kimoja pekee cha maji ambacho hakikuweza kusitiri uhai wao. Hivyo, Nakuruto aliwasihi na kuwashauri wachimbe visima na mabwawa ya maji pale Maweni. Aliwarai wafanye hima ili wapate maji ambayo ni uhai wao kisha wayatumie kwa ukulima na ufugaji wa mifugo. Anawaeleza kuwa, baada ya miti kumea na misitu kuchipuka na kusitiri maji, mvua ingenyesha kwa wingi na hivyo hawangehitaji visima tena. Mazingira nadhifu hukidhi mahitaji na haja ya jamii kwa hali na mali. Kwa mfano, Momanyi katika riwaya yake anasema kuwa,

> "Maji yalifoka kwenye visima, miti ikachipuka, mvua zikanyesha na kujaza mabwawa ya maji. … Nchi ilipiga kijani kwa wingi wa maji, mikuza ikang'ang'ania nafasi huku mimea ya kila aina ikipandwa. … Mazizi ya ng'ombe yalijaa na bubujiko la nyemi likachanua kwenye nyuso za Wamaweni na kufukuza ulitima" (uk. 72).

Hili ni dhihirisho kuwa, mazingira yana uwezo mkubwa wa kufukuza ulofa yakihifadhiwa vyema. Utandawazi katika mataifa mengi barani Afrika huweza kuzalisha uhuluti wa utamaduni, lugha na itikadi za jamii. Mathalani, kutokana na athari za utandawazi, mna barabara inayoitwa *Spider Road*, jengo liitwalo *Snow Crest* na mkahawa uitwao *Vivid Dreams Restaurant* katika mji mkuu wa Maboni.

Hili ni dhihirisho kuwa mazingira ya Waafrika yamenajisiwa na viongozi wa mataifa ya Ulaya na Uropa, kiwango kwamba Waafrika wengi huzionea fahari lugha za kigeni na kuzidharau zao mame ati ni duni. Viongozi wazalendo kama Nakuruto wanashangaa na kujiuliza ikiwa Afrika itachomokewa na jua la ufahamu na uzalendo. Nakuruto anauliza kama itawadia siku ya halafu, Waafrika waache kutumia majina ya kigeni kama yale ya akina Quick Buck kwenye barabara na majengo. Majina haya huwakumbusha Waafrika enzi za jinamizi – Wakoloni.

Utandawazi unaathiri tamaduni za Waafrika kwa kiwango kikubwa. Mathalani, mna pepo zinazovuma na kuathiri vijiji tofauti tofauti. Vijiji hivi vinaashiria mataifa mengi fukara barani Afrika. Vijiji hivi viliathirika na vikakumbatia na kuziruhusu pepo zile ziathiri mienendo na hulka yao. Kwa mujibu wa mwandishi pepo hizi zilitoka upande wa magharibi. Upande wa magharibi unaashiria mataifa tajiri ya Magharibi. Katika hali hii, baadhi ya tamaduni za wanavijiji zilipeperushwa na upepo na kuwapelekea wanakijiji kuiga mambo ya kiajabuajabu yasiyokuwa na uasili wa maisha yao. Baadhi ya tamaduni zilisahaulika na zingine kubadilika kabisa. Kutokana na tamaa ya kutajirika, watu wengi wanakuza mimea kutoka ughaibuni kwa kisingizio kuwa vyakula vya Waafrika vya kiasili havina madini na virutubishi. Ukweli ni kwamba, tuhuma hizi husambazwa na mataifa ya Ulaya na Uropa yanayopania kutawala mataifa ya Afrika kupitia vikaragosi wanaochaguliwa na wananchi. Umaskini unapaliliwa pale udongo unapotoholewa ili uzalishe mazao ya ughaibuni. Kadhalika, wanavijiji waliacha kukuza mimea iliyohimili mazingira ya asili yao na kukuza ile ambayo haikukubali mazingira ya Afrika.

Ubinafsi na tamaa zilizalisha chuki, ghadhabu na hatimaye, uharibifu wa mali asilia. Momanyi anaeleza kuwa, chuki na ghadhabu vilishamiri, kutanda na kutawala mioyo na nafsi za wanavijiji. Anaongeza kuwa, ubinafsi uligubika ujamaa na undugu na badala yake hasira na kiburi vikanawiri. Uharibifu nao ulizaliwa. Uharibifu hasa wa mali asili ulielekea kuitia dunia najisi ishindwe kuzalisha na kuhimili maisha ya viumbe wote. Hata hivyo, ni vyema kukumbuka kuwa, kama vile Momanyi anavyoshauri, utando unaonasa mataifa fukara ya Afrika unahitaji ujuzi wa kiutandawazi ili kumaizi namna nyavu zake za ndani zilivyotandazwa kuuteka nyara uchumi wa Afrika.

**Maadili ya Mazingira**

Nanda (2012) anajadili kuwa, ingawa binadamu ana mamlaka ya kuyadhibiti na kuyatawala mazingira kwa jumla, mazingira yenyewe yana haki. Hivyo, ni haki ya mazingira kutunzwa na binadamu. Howarth (1996) anaongeza kuwa, binadamu hukiuka maadili ya mazingira kwa kuwa ndiye chimbuko la upujufu wa mazingira ulimwenguni. Hivyo, binadamu hajafanikiwa kuyalinda, kuyahifadhi na kuyasimamia mazingira dhidi ya ukiukaji wa maadili ya mazingira. Hili limenawirishwa na haja na ubinafsi wa binadamu wa kutumia rasilimali mbalimbali duniani zinazozalishwa na mazingira bila kuzingatia maadili ya mazingira (Baek, Cho na Koo 2009). Momanyi anatahadharisha kuwa maingiliano kati ya binadamu na mazingira yaongozwe na yajikite katika misingi ya maadili ya kimazingira. Mathalani, mhusika ba Ludao analalamika kuwa ziwa Ipe halitoi samaki kutokana na gugumaji lililotatiza uvuvi. Ikizingatiwa kwamba uvuvi ndicho kitega uchumi katika eneo la ziwa Ipe, samaki walipohama ukame ulikita mizizi na kufana sana. Maij nayo yalipungua kwa kiwango kikubwa. Ukame uliwafukuza wanakijiji wa eneo lile wakahamia mjini Maboni. Nakuruto anawakumbusha ba Ludao na ba Chande kuwa wanakijiji ndio waliosababisha samaki kuhama kwa sababu hawakutunza mazingira ya ziwa Ipe. Mathalani, babu mkuu wa ba Ludao ndiye aliyeanzisha uchimbaji wa mitaro na kuyafuja maji ya ziwa kunyunyizia mashamba yake. Nakuruto anawakumbusha ba Ludao na ba Chande kuwa ni jukumu lao kuharibu gugumaji lile kabla liangamize ziwa pamoja na wenyeji.

Kwa upande mwingine, wanakijiji wa kijiji cha Latimbi waliyapuuza mazingira yao bila kuyalinda na kuyahifadhi. Kima cha maji ya mto Milu kilishuka ukabaki kijito tu. Hapo kabla, mto Milu ulikuwa unarindima kwa wingi wa maji na kunawirisha kijiji kizima cha Walatimbi. Wanakijijji walifyeka misitu na mahala pake pakabaki visiki vyeusi. Misitu ambayo hapo zama zile za shibe, umoja na amani ilisheheni aina chungu nzima za miti ya kiasili kama vile anavyoeleza Nakuruto. Kwamba ilisheheni mivule, mikuyu, mipingo na mibambakofi. Janibu zile sasa ziligeuka kuwa

tambarare lililozagaa visiki na vijumba vya mafukara. Hili ladhihirisha kuwa, uhusiano mwema wenye maadili kati ya binadamu na mazingira hufukuza ulofa na kukemea ukame, ilhali mbaya usio na maadili mema hupalilia ukame, ulofa, hasira, chuki na maafa.

Kadhalika, mashamba makubwa yaliyokuwa yakizalisha vyakula vya kiasili kama mawele, mtama, machungwa na maboga yaliadimika kutokana na utovu wa maadili ya mazingira baina ya Walatimbi. Miembe michache iliyokuwa mle pamoja na vibanda vichache ndivyo vilivyosalia kama ushuhuda kuwa mliwahi kuwa na mashamba mle. Vijumba vilivyoezekwa kwa makuti na vilivyositiri nyuso zilizosinyaa kwa kukosa lishe bora vilihanikiza maeneo yale. Wanakijiji ambao waliwahi kumfukuza Mbeberu na kuishi kwa umoja na shibe baada ya kugawanya shamba lililowahi kutawaliwa na Bw. Brook baina yao wenyewe, waligeuka waombaji. Walatimbi waliowahi kuteka maji kutoka mto Milu kwa shangwe na vigelegele walisalia na maji yaliyokuwa karibu kuwa tope. Walatimbi ambao waliwahi kuvuma kwa uhai walijitosa kwenye maisha yaliyofurika kifuu kitupu, bila matumaini ya kesho yenye heri. Vijana Walatimbi waliojivunia mazingira na hasa mifugo yao wakahamia katika vijiji jirani. Walatimbi ambao wakati mmoja, njaa na uhitaji vilitengana kabisa nao na badala ya ukame wakashakiri na kutononoka kwa wingi wa shibe, walijizatiti kuchafua mazingira. Uchafuzi ule uliwatumbukiza na kuwazamisha katika bahari ya ufukara. Walatimbi waliopalilia miti iliyochipuza uhai, walielekea kuangamizwa na njaa, kiangazi, mifumo ya uongozi dhalimu na uchochole.

Tamaa na ubinafsi wa binadamu inamfanya asahau maadili mema ya mazingira. Uchafuzi wa mazingira unaotokana na mbio za walafi za kujitajirisha wao bila kujali wanakijiji unasababisha kukauka kwa mto Milu. Uchafuzi ule ulijumuisha uharibifu wa miti iliyositiri kingo za mto Milu pamoja na uchimbaji wa visima uliozalisha kushuka kwa kima cha maji ardhini. Ukosefu wa miti unachangia ukosefu wa mvua ambao unazalisha ukame. Unajisi wa mazingira unachangia Walatimbi kuinyonya rutuba na kuiacha isombwe na maji ya mvua ovyo. Aidha, utovu wa maadili mema kati ya binadamu na mazingira unachangia maafa. Nakuruto anasema kuwa, kijiji cha Latimbi kilipungukiwa na idadi ya watu na vijana walioelimishwa kutokana na upungufu wa mavuno ya ardhi na hili lilipelekea wao kuhamia vijiji vingine. Ardhi iliyochipuza uhai wa Walatimbi sasa imegeuka kuwa jangwa yabisi lisiloweza kuzalisha hata kwekwe.

Utovu wa maadili mema ya mazingira ulichangia mabadiliko hasi katika kijiji cha Maweni. Eneo lililosheheni watu wenye bidii katika kilimo liligeuka mahame. Katika janibu zile, ardhi ililimwa, watu walisomba mazao kwenye maghala na mabohari, wengine kutoka vijiji jirani walimiminika Maweni kununua mazao ya kila aina, na pia Maweni kilisheheni masoko makubwa yaliyotumiwa nao kuchuuzia mazao yao na kujizolea faida tele. Lakini sasa kilibaki mahame tu. Ghala kubwa lililowahi kuhifadhi nafaka hapo kabla ili kusubiri wanunuzi lilifura na kuhanikiza uvundo hadi nje ya jengo kutokana na marundo ya taka yaliyorundikana mle. Kuta za jengo lile ziligubikwa na vumbi zito la hudhurungi. Ng'ende, mijusi na buibui walistarehe kila eneo mle ndani wakihadithiana walizozifahamu na zilizowakwepa. Sakafuni, magwaride ya panya wadosi yalipishana kwa heshima na taadhima ilhali wanyonge walizozana kwenye milima ya taka wakisaka tonge.

Aidha, visima vichache vilivyochimbwa, hatimaye, viligeuzwa kuwa mashimo ya kutupia takataka punde tu vima vya maji vilipopungua. Hizi zilikuwa athari hasi za mahusiano yaliyokosa maadili mema kati ya Wanamaweni na mazingira yao. Kwa mfano, Nakuruto kutokana na huzuni inayomvaa punde anaposhuhudia uharibifu wa mazingira, katika kijiji cha Maweni anajiuliza kibalagha kuwa, "Udongo huu haungesitiri uhai. Watu walifaidi rutuba yake kwa miaka mingi bila kuurutubisha, vipi ungewapa mazao?" (uk. 118). Eneo lililowahi kufoka maji kwenye visima sasa lilikauka kweli. Eneo lililochipuza miti na mvua kujaza mabwawa ya maji lilikuwa na kisima kimoja tu kilichosalia kutosheleza mahitaji ya kijiji. Nchi iliyowahi kupiga kijani kwa wingi wa maji na mikuza ikang'ang'ania nafasi, sasa iliota vibanda pamoja na vijumba vidogovidogo mithili ya uyoga. Nchi iliyowahi kupendeza iligeuka kero kutokana na vichochoro vilivyohanikiza uvundo uliotokana na maji taka yaliyomwaika ovyo kutoka katika vibanda.

Maadili mema ya mazingira huwawezesha watu kujitambua wao wenyewe kwa kufahamikiwa wao ni nani, asili yao na wanatoka wapi. Hili huwakumbusha haja ya kuhifadhi mazingira kupitia maadili mema ya mazingira. Kwa mujibu wa Momanyi, utovu wa maadili mema ya mazingira baina ya watu, huzalisha ulitima na utegemezi wa misaada kutoka mataifa ya Ulaya na Uropa badala ya kujitegemea. Hata hivyo, Nakuruto anahimiza kuwa uhusiano wenye maadili mema kati ya binadamu na mazingira huzaa matunda matamu na mabivu baada ya uvumilivu. Mathalani, anamwambia Ngocho kuwa, "Ngocho, ukitaka mawaridi, vumilia miiba" (uk. 112).

**Hitimisho**

Mwandishi anasisitiza kuwa, suluhu za changamoto zinazoyakabili mataifa fukara barani Afrika, hasa za kimazingira zimo mumu humu Afrika ila sio ughaibuni. Hata hivyo, anatahadharisha kuwa, ikiwa ubinafsi, tamaa na ufisadi ambao ni watoto wa ufukara hawataangamizwa, basi daima Waafrika watasalia kuwa vibaraka wa Ulaya na Uropa. Uchafuzi wa hewa ni kizingiti kikubwa katika kunadhifisha mazingira, kwani wengi huaga kutokana na nduli zinazosababishwa na uchafuzi huu. Hivyo, mwandishi anasisitiza haja ya kulitatua tatizo hili kabla ya kuyaangaza mengine. Mataifa fukara barani Afrika, hujipata yakitapatapa katika gereza la mikopo yenye riba ya juu na masharti magumu yasiyoweza kuyamudu, kutoka mataifa ya Ulaya na Uropa. Ndiposa mwandishi anasisitiza umuhimu wa bara la Afrika kwa jumla kujitegemea na kusuluhisha dhiki zote kwa kunadhifisha mazingira na kuyatawaza najisi yaliyopata kutoka ughaibuni. Anahitimisha kwa kushauri kuwa, najisi ya mazingira ya Afrika kutoka kwa mataifa tajiri ya Ulaya ndiyo iliyozalisha aina zote za maradhi, dhambi za kila aina na masumbufu mengi yanayowaathiri Waafrika hadi leo. Hii ndiyo maana, anasisitiza haja ya Waafrika kudumisha utamaduni wao ambao huchangia pakubwa katika uhifadhi wa mazingira asilia – badala ya kuuchukua na kuuenzi ule wa Magharibi unaopofusha bila kudadisi umuhimu na athari zake dhidi ya Waafrika. Cha msingi, anawarai Waafrika wayasuluhishe matatizo yanayowakumba kwa kuyahifadhi mazingira yao wenyewe bila kuiga mbinu za Wazungu, kwani changamoto za Kiafrika zinahitaji kutatuliwa katika mazingira ya Kiafrika; mawazo ya Kiafrika na mikakati ya Kiafrika. Ingawa anasisitiza haya, anaonya dhidi ya kupuuza mbinu za kisasa katika kuyanadhifisha na kuyahifadhi mazingira. Anawarai Waafrika wasididimizwe na mapazia ya wakati katika kuhifadhi mazingira yao. Kwa misingi hiyo hiyo, anasisitiza umoja baina ya Waafrika ili wasije wakatawanywa na watawala wa mataifa tajiri ya Ulaya na Uropa. Hatimaye, anasadiki kuwa maji, hewa na udongo barani Afrika ndiyo uhai wa Afrika.

**Marejeleo**


Baek, J., Cho, Y. & Koo, W. W. (2009). The Environmental Consequences of Globalization: A Country-Specific Time –Series Analysis. Ecological Economics, pg. 68 (8 - 9), 2255- 2264

Garrard, G. (2004). *Ecocriticism*. Routledge: Tylor & Francis Group, New York: USA.

Glotfelty, C. na Fromm, H. (Eds.). (1996). *Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. Athens and London: The University of Georgia Press.

Heise, U.K. (Mh.) (2016). *Literatures, Cultures and the Environment*. Palgrave: Macmillan.

Howarth, B. R. (1996). Climate Changes and Overlapping Generations. *Journal of Contemporary Economic Policy, 14(4). Pg. 100-111.* https://doi.org/10.1111/j.1465 -7287.1996.tb00637.x

Kusserow, K. (2018). "Welcome Remarks." *Picture Ecology: Art and Ecocriticism in Planetary Perspective Symposium*. Princeton University: Princeton University Press, December, 7.

Mhango, P. na Bulaya, J. (2022). Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. *MULIKA Na. 38*, uk 105 –125.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi, Kenya: Sasa Sema, Longhorn Publishers Limited.

Morton, T. (2012). *The Ecological Thought*. Cambridge, MA: Havard University Press.

Mwaniki, J. M. (2019). 'Athari za Mtagusano kati ya Jamii na Ekolojia Katika Ushairi wa Kithaka Wa Mberia: Bara Jingine na Rangi ya Anga'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachaishwa).

Nanda, V. P. (2011). *Climate change and environmental ethics*. New Jersey: Transaction Publishers.

Nayar, K. P. (2010). *Contemporary Literary and Cultural Theory: From Structuralism to Ecocriticism*. Delhi, India: Longman.

Ntarangwi, M. (2004).*Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Islands. Augustine college.

Robert, T.T. & Christine, M. B. (Eds.). (2016). *Ecocriticism and Geocriticism: Overlapping Territories in Environmental and Spacial Literary Studies*. New York, NY: Palgrave Macmillan.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*.Nairobi. Oxford Press Nairobi, Kenya.

Waithiru, A. K. (2019). 'Matumizi ya Taashira Kuangaza Jiografia na Utandawazi Katika Tamthilia za *Zilizala* na *Sudana'*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Laikipia (Haijachapishwa).

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

_____________ (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publisher.